JIMBO KATOLIKI DAR ES SALAAM

UONGOZI WA PAROKIA TEULE YA MTAKATIFU BENEDICTO - ABATE - UTETE



Padre Francis Malele



Joseph N. Magati



Teddy J. Mwandika



Ambrose Monyiaichi



Monica W. Vitalis

MWAKA 2017 - 2019



Salvatory Callist



Joseph D. Mwijoba

JIMBO KATOLIKI DAR ES SALAAM

UONGOZI WA PAROKIA TEULE YA MTAKATIFU BENEDICTO - ABATE - UTETE

MWAKA 2020 - 2023



Father Francis Pastory Malele

Msimamizi Parokia Teule - Utete



Ndg:-Joseph Damian Mwijoba

Katekista Parokia Teule - Utete



Ndg:-Joseph Nathanael Magati

Mwenyekiti Parikia Teule - Utete



Ndg:-Monica Wahindi Vitalis

Katibu Parokia Teule - Utete



Ndg:- Tedy Joseph Mwandiki

Mwenyekiti Msaidizi Parokia Teule Utete



Ndg:- Salvatori Calist Ndaskoi

Mtunza Hazina Parokia Teule Utete



Ndg:- Michael Machibya Katibu Msaidizi Parokia - Teule Utete

HISTORIA YA POROKIA TEULE YA MTAKATIFU BENEDICTO ABATE UTETE.

UTANGULIZI

Jitihada ya kujengwa kwa kanisa la Utete ilianza mwezi Juni 1965 kupitia Mganga mkuu wa Hospitali ya Wilaya Utete Dr. Kasambala. Jitihada hizo zilianza baada ya Mganga Mkuu Kumpokea mgojwa aliyetokea kilwa Kipatimo Marehemu Mr Kilindo. Wakati wa kumhudumia mgojwa huyu, mgonjwa alifikia wakati akaomba huduma ya padre hasa ubatizo. Dr Kasambala kwa wakati huo hakuweza kumpata padre ambaye angeweza kumpatia mgojwa sakramenti kama ilivyokuwa kiu ya mgojwa. Hii ilitokana na sababu hapakuwepo na kanisa katoliki eneo la Utete wala padre.

Mganga mkuu aliwakusanya waumini Wakristo waliokuwepo wakti huo wakitoa huduma mbalimbali ya matibabu kwenye Hospitali na kuwaomba kusali pamoja na mgojwa kama njia ya kumfariji mgonjwa kulingana na kiu yake ya kupata huduma ya kiroho. Baada ya kumaliza sala ya pamoja wakiwa na Mr Kilindo kwa bahati mbaya mgonjwa alipoteza maisha na waumini hao wachache kugubikwa na machozi pamoja na maombelezo ya kumpoteza mgojwa wao.

Kutokana na tukio hilo, Dr. Kasambala alianza jitihada ya kujenga kanisa kwenye eneo la Utete. Mnamo mwezi Oktoba 1965 ilitokea bahati nzuri Hospitali ya Utete kutembelewa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Katika risala ya Utii kwa Mheshimiwa Rais wa Tanzania Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, Dr.Kasambala alimuomba Rais awapatie eneo kwa ajili ya kujenga kanisa ili Wakristo wapate sehemu ya kusali. Rais katika kujibu risala alimuagiza Mganga mkuu atoe aneo la Hospitali ili lijengwe Kanisa. Hali hiyo ndiyo ilipelekea kupatikana kwa kiwanja ambapo kanisa limejengwa.

UJENZI WA KANISA UTETE

Ujenzi wa kanisa la Utete ulianza mapema mwaka 1966 na kupitia kwenye nyakati tofautitofauti ambapo kanisa hii ilijengwa na kubomolewa mara nyingi na wananchi wanaoishi katika eneo ili la Utete. Kubomolewa huko kwa jengo la kanisa iliyokuwa inajengwa ilitokana na wananchi kutokuwa tayari kujengwa kwa kanisa kwa vile wao walikuwa na imani tofauti (yaani Waislamu).

Harakati wa ujenzi iliongozwa na na Padre Robin wa kanisa na Anglican aliyekuwa akitoa huduma kwenye kituo cha wakoma kwenye kitongoji cha Kidwitwi. Ujenzi wa kanisa ilikamilika baada ya miaka 3, hii ina maana mnamo mwezi Juni 1969 ujenzi wa kanisa hili ulikamilika na waumini kupata sehemu ya kusali karibu na maeneo yao ya kazi (karibu na Hospitali ya Wilaya)

Kwa mara ya kwanza huduma ya Ibada ilikuwa inatolewa na Padre Robin wa kanisa la Anglikan. Kutokana na kukua na kuongezeka kwa waumini na baada ya taarifa kuenea juu ya upatikanaji wa waumini wakatoliki katika eneo la Utete, Mapadre wa kanisa katoliki kutoka kilwa kipatimo alikotokea marehemu Mr. Kilindo walianza kuja kutoa huduma ya kiroho. Usafiri pekee iliyokuwa ikitumiwa na mapadre hao ilikuwa ni usafiri wa trekta kutoka kilwa hadi utete. Hii ilikuwa ni kwenye miaka 1975 hadi kwenye miaka ya 1980.

Baada ya mapadre kutoka kipatimo kuacha kuja kutoa huduma ya misa ikaanza kutolewa na mapadre kutoka Mbagala Dar es salaam. Hali hii iliendelea kwa muda mrefu hadi mwaka 1997 ilipaanzishwa parokia ya Kibiti. Baada ya kuanzishwa kwa Parokia ya kibiti, na kanisa la utete kuwa miongoni mwa vigango vya Parokia ya Kibiti huduma ya kiroho kwa waumini iliendelea kuimarika kwa maana sasa huduma ya misa iliweza kupatikana mara kwa mara kwa vile mapadre walikuwa hawapo mbali saana ukilinganisha na wakati huduma hii ilipokuwa ikitolewa na mapadre kutoka Kilwa au Mbagala.

Mnamo mwaka 2014 Kigango cha Ikwiriri, iliyokuwa miongoni mwa vigango vya Parokia ya Kibiti kutangazwa kuwa Parokia, Kigango cha Utete Kkikawa miongoni mwa vigango vya Parokia Teule ya Ikwiriri.

Mchakato wa kukua kiimani kwa waaami wa eneo la Utete haikuishia hapo, kwani mnamo tarehe 7/7/2018 Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo Askofu Mkuu wa kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es salaam alitangaza kigango cha Utete kuwa Parokia Teule na Padre Francis Pastory Malele kuteuliwa kuwa msimamizi wa Parokia Teule ya Mtakatifu Benedicto Abate Utete.

Ili kumuwezesha paroko Mteule kuishi Utete, Waamini kwa pamoja walikuwa na jukumu la kutafuta nyumba ya kupanga ambapo walifanikiwa kupata Nyumba ya Ndugu Wamara Chaurembo. Nyumba hii ilihitaji ukarabati Mkubwa kazi iliyofanyika kwa nguvu/michango ya waamini wa Utete na baadaye kupata msaada kutoka Parokia ya Kunduchi walipewa na jimbo kazi ya kulea parokia Teule. Uongozi wa parokia ya Kunduchi, walisaida jumla ya **Tsh 2.400,000.00** zilizotumika kukamilisha suala la ukarabati. Nyumba anapoishi Paroko Mteule ni kama inavyoonekana hapa chini



Nyumba ya kupanga kwa ajili ya makazi ya muda ya Paroko Mteule Padre Francis Pastory Malele 2019

Baada ya kutangazwa kwa Parokia Teule, uongozi wa Jimbo ulitangaza mipaka kati ya Parokia ya Ikwiriri na Parokia Teule ya Utete kuwa ni Mto Rufiji. Aidha, Padre Francis Pastory Malele alitangazwa kuwa msimamizi wa Parokia Teule - Utete. Kwa huo mpaka, vigango vinavyounda Parokia Teule ya Utete ni pamoja na Kigango Mama cha Utete, Kigango cha Nambunju na Kigango cha Mohoro.

Maeneo mengine yenye nafasi ya kuanzishwa vigango ni pamoja na Kiwanga, Chumbi, Nyamwage, Mbwara, Tawi, Utunge na Ngarambe. Aidha, Jumuiya mbili zinapaswa kuanzishwa kwenye kitongoji cha Siasa (Nyamakurukuru) na Nyawanje (Ngwembele) na kujumuishwa kwenye kigango cha Utete. Kwa mwaka 2019 Vigango vya Parokia Teule ya Utete ni pamoja na Kigango cha Utete, Nambunju na Mohoro .

KIGANGO CHA UTETE

Kigango cha Utete ina jumuiya sita (Mt.Paulo, Mt. Secilia, Mt Yuda Thadei, Mt. Joseph, Mt.Therecia na Jumuiya ya Kristo Mfalme. Jumuiya zote zina Familia hamsini na saba (57) na wumini miambili na sita (206).

JUMUIYA YA MTAKATIFU MT.PAULO,

Jumuiya ya Mtakatifu Mt. Secilia

Jumuiya ya Mtakatifu Therecia

Jumuiya ya Kristu Mfalme

KIGANGO CHA MOHORO

Kigango cha Mohoro kina jumla ya Jumuiya tatu ambao ni kama ifuatavyo

Jumuiya ya Mt. Therecia wa Mtoto Yesu

Jumuiya ya Mt. Petro na Paulo

Jumuiya ya Aloisi Gonzaga

Jumuiya ya Mt. Yohana

KIGANGO CHA NAMBUNJU

Kigango cha Nambunju kina jumla ya Jumuiya tatu kama ifuatavyo

Jumuiya ya Mt. Petro

Jumuiya Ya Mt. Ambrosi

Jumuiya Ya Mt. Theresia

UONGOZI WA PAROKIA TEULE TENGU KUANZISHWA

Parokia Teule ulianza kama kigango cha Utete kwenye miaka 1969 ikiwa ni kanisa la umoja wa makanisa ya Kilutheri, Anglican na Katholiki. Katika kipindi hicho kwa upande wa wakatoliki, kigango kilikuwa chini ya jimbo la Masasi na kwa maana hiyo mapadre walikokuwa wanatoa huduma japo mara moja kwa mwezi walikuwa wanatoka Kilwa kipatimo kwa usafiri wa trekta. Ilipofika mwanzoni mwa miaka ya themanini, kigango kiliamia jimbo la Dar es salamaa na mapadre walioukwa wanakuja kutoa huduma walikuwa wanatokea Mbagala.

Padre wa kwanza mwanzilishi anaitwa Father Robin wa kanisala Angilikana akitokea kituo cha kulelea wagonjwa wa ukoma Kindwitwi, baada ya pardre Robin, mapadre waliofuatia walitoka Kilwa kipatimo na baadaye Mbagala.

Kigango cha Utete kimekuwa kwenye uangalizi wa parokia ya Kibiti kati ya mwaka 1997 hadi mwaka 2014. Aidha mnamo mwaka 2014 Parokia ya Ikwiriri ilianzishwa na Utete kuwa moja ya vigango vyake. Usimamizi ulibadilika kutoa kwa fether Christian Lupindu na Kuwa Dismas Kimboi. Mnamo mwaka 2018 Mhadhama Kardinal Polycarp Pengo alitangaza kigango cha Utete kuwa Parokia Teule na kumteua Father Fransis Malele kuwa Paroko Mteule. Hii ina maana tangu kuanzishwa kwa parokia Teule ya Utete Mapadre walitoa huduma ya kiroho ni kama ifuatavyo.

S/NO	JINA LA PAROKO	MUDA WA UONGOZI
1	Father Christian Lupindu	1997 - 2014
2	Father Dismas Kimboi	2014- 2018
3	Father Francis Pastory Malele	2018 kuendelea

Usimamizi wa kiroho kwenye Parokia haiwezi kukamilika kama hakuna wasaidizi, kwa kawaida wasaidizi wa Paroko ni Makatekista. Tangu Kigago cha Utete hadi kufikia kutangazwa kuwa parokia Teule, makatekista walifanikiwa kutoa huduma ni pamoja na

S/NO	**JINA LA KATEKISTA**		**MWAKA WA HUDUMA**
1	Wiliamu Njimbwi	-	1979 -1995
2	Yohana Mpalakele	-	1995 -1996
3	Lucas Ng’ambu	-	1996 - 2006
4	Sylvesta Mtupa	-	2006 - 2010
5	Joseph Mwijoba	-	2010 hadi sasa

VIONGOZI WA KIGANGO CHA UTETE KABLA YA KUWA PAROKIA TEULE.

Baadhi ya viongozi waliosimamia kigango cha Utete baada ya kuanzishwa kwa Parokia ya Ikwiriri ni pamoja Mr Revocatus Nandi Mwenyekiti, Mwalimu Adinan Mwenda Katibu Msaidizi Mr Kilindo Katibu, Joachim Nyaligo Katibu Msaidizi na Mama Ansila Makilikila Mtunza Hazina.

Baada ya kuanzishwa kwa Parokia Teule ya Utete viongozi waliochaguliwa ni kama ifuatavyo:-

S/NO	JINA KIONGOZI		WADHIFA
1	Mr Joseph Nathaniel Magati	-	Mwenyekiti,
2	Dr Tedy Mwanditi	-	Makamu Mwenyekiti
3	Mwalimu Monica Vitalis	-	KATIBU
4	Mr Ambrose Monyiaichi	-	KATIBU MSAIDIZI
5	Mr Salvatori Calitus Ndaskoi	-	MTUNZA HAZINA

Viongozi hawa wameongoza kiganga ukiwa ni miongoni mwa vigango kwenye parokia ya Ikwiriri na baada ya kigango cha Utete kutangazwa na Mhadhama Kardinal Polycarp Pengo kuwa Parokia Teule.

MATUKIO MBALIMBALI YA KIHISTORIA NDANI YA KANISA KATOLIKI PAROKIA TEULE YA UTETE.

1. Mwaka 2013 Misa ya kuweka Jiwe la Msingi nyumba Mapadre iliadhimishwa na Askofu Msaidizi wa kanisa katoliki Jimbo Kuu Dar es salaam mhashamu Mdoe.
2. Tarehe 04/07/2018 Mhadhama Polycarp Kardinal Pengo alipandisha hadhi kutoka kigango kuwa Parolia Teule ya Utete kwenye misa ya upadirisho iliofanyika Msimbazi center na Father Francis Malele kuteuliwa kuwa Paroko Mteule wa Parokia Teule ya Mtakatifu Benadicto Abate Utete.
3. Mwaka 2018 Wanaume wakatoliki (UWAKA) walifanya ziara ya kiuchungaji iliyopelekea kupatikana kwa **Tsh 13,500,000.00** iliyosaidia kuchimba kisima kwa ajili ya kupata maji kwa maendeleo ya kanisa
4. Mwaka 2018 Porokia ya Kunduchi walitembelea Parokia Teule kama walezi na kufanikisha kutoa msaada wa **Tsh 2,400,000** iliyosaidia kumaliza ukarabati wa nyumba analihishi Paroko kwa sasa. Mwaka 2018 kwaya ya Mtakatifu Benateda yenye washiriki 24walitembelea parokia Teule kwa ajili ya kuinjilisha.
5. Mnamo tarehe 27 hadi 30/06/2019 Ziara ya Utoto Mtakatifu kutoka jimbo Kuu Dar es salaam walitembelea Parokia Teule ya Utete kwa lengo la kuinjilisha ambapo jumla ya washiriki 1462 wakiongozwa na Baba Mhadhama Kardinali Porlicarp Pengo aliyetembelea Utete kwa mara ya pili baada ya miaka 38. Katika uinjilishaji huo matukia muhimu yaliyofanyika ni pamoja na
    i. Kusherekea miaka 48 ya Upadre wa **Mhadhama Kardinali Polycarp Pengo**.
    ii. Kusherekea miaka 50 ya Ukristu Utete, sanjari na miaka 50 ya Halmashauri ya Walei Jimbo Katoliki Dar es salaam.
    iii. Kubatizwa kwa watoto 13 wadogo.
    iv. Waliopata Sakramenti ya Kipaimara walikwa 8 wakiwemo wanandoa 3.

v. Pia Jozi tisa (9) za ndoa zilifungwa

Picha mbalimbali ya matukio kadhaa yaliyojitekeza kabla na baada ya Utete kuwa parokia ni kama yanavyooneka hapo chini.



Father Fransis Pastory Malele akiwa kwenye misa takatifu Parokia Teule Utete mwaka 2019



Viongozi Teule wakiwa kwenye tathmini eneo la ujenzi wa nyumba ya mapadre 2019



Legio Maria kutoka jimboni wakiwa kwenye misa Parokia Teule Utete mwaka 2019



Legio Maria kwenye picha ya pamoja Parokia Teule - Utete mwaka 2019



Utoto Mtakatifu kwenye zoezi la kupeleka shukrani wakati wa misa takatifu mwaka 2019